

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

SIMU NA :027-2530022

2530042

NUKUSHI NA

:027/2530022

:027/2530042



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
(W),
S.L.P. 2,
KATESH-HANANG,
MANYARA.**

04/06/2021

TANGAZO LA UKODISHAJI WA VIBANDA VYA STENDI YA KATESH

NA SOKONI. (LIMEONGEZWA MUDA)

ZABUNI NA. LGA/059/2021/2022/NC/04

Kwa mujibu wa kanuni ya 13(5) ya kanuni za manunuzi ya umma za mwaka 2013 pamoja na marejeo yake ya mwaka 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang **imeongeza Muda wa siku 7 kuanzia tarehe 8/6/2021 hadi tarehe 14/6/2021.** Hivyo inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa vibanda vya Biashara vilivyopo Stendi ya Mabasi Katesh na Soko kuu la Katesh.

MASHARTI YA ZABUNI YA UKODISHAJI WA VIBANDA


Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo kamili na vivuli vya nyaraka zilizothibitishwa.

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 20,000/= kwenye benki ya NMB baada ya kupewa Bill na Idara ya Fedha na Biashara ambayo haitarudishwa hata kama mwombaji wa Zabuni hatateuliwa. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 08/06/2021 hadi tarehe 14/06/2021.
2. Mwombaji wa zabuni anayetarajia kufanya biashara kwenye Kibanda atalazimika kubandika picha yake ya sasa kwenye kiboma kilichopo kwenye kablasha la zabuni. Mwombaji yeyote atakayeshindwa

kufanya hivyo maombi yake hayatafikiriwa kwenye tathimini atakuwa amejiondoa moja kwa moja.

3. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa mwaka moja tu.
4. Mwombaji wa Kibanda atalipa dhamana ya kodi ya Mwezi mmoja.
5. Mwombaji wa Kibanda ndiye atakuwa mpangaji wa kibanda husika.
6. Mwombaji wa kibanda haruhusiwi kupangisha mtu mwingine yeyote "Subrenting".
7. Mwombaji atatakiwa kulipa ada ya usafi wa mazingira ya mwaka sawa na Tshs.12,000 ambayo italipwa kabla ya kukabidhiwa Kibanda.
8. Mwombaji asiwe na deni lolote katika Halmashauri ya wilaya.
9. Mwombaji wa Kibanda aambatanishe Namba ya Mlipa Kodi (TIN) pamoja na cheti cha utakaso cha mlipa kodi(Tax Clearance Certificate)
10. Kodi ya kibanda italipwa kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu na mpangaji atatakiwa kulipa kodi kabla ya tarehe 25 ya mwezi unaoanza kulipa awamu nyingine.
11. Kodi ya vibanda vya sokoni niTsh.20,000/= na Stendi ya Mabasi Katesh ni Tshs.50,000/= tu kwa kibanda.
12. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kuwa na Leseni hai ya Biashara anayoenda kufanya kwa kutumia kibanda hiko.
13. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atapaswa kutunza Jengo na kuweka mazingira kuwa safi wakati wote na kuikabidhi kwa Halmashauri ikiwa katika hali nzuri.
14. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atahusika na uharibifu au hasara yoyote itakayojitokeza katika utumiaji na utunzaji wa majengo hiyo wakati ikiwa ndani ya muda wa mkataba.
15. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kulipa gharama zote za umeme na maji katika kibanda anachotumia.
16. Mwombaji wa zabuni atakayeshinda akikiuka kulipa kodi ya kibanda kujaza mkataba kwa wakati uliopangwa atanyang'anywa kibanda hicho.
17. Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.

- Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:
KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,
S.L.P 2,
KATESH – HANANG.
 - Juu ya bahasha iliyofungwa vizuri iandikwe ZABUNI YA UKODISHAJI WA VIBANDA VYA STENDI YA MABASI KATESH AU SOKO KUU KATESH.
18. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya jumatatu tarehe 14/06/2021 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.
- Maombi ya zabuni ambayo hayataletwa na kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubalika.


SOLOMON I SHATI
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

NAKALA:

1. Ofisi ya Katibu Tawala Wilaya Hanang'
2. Watendaji wa Kata - Wajulisheni Watendaji wa vijiji na wananchi katika Kata zenu
3. Mbao za Matangazo